# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 033 SEPTEMBA 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



1 WATAFITI WASISITIZWA USHIRIKI JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIA NCHI

2 WADAU WAKUTANA KUJADILI MPANGO KAZI WA UWEKEZAJI WA MIUNDOMBINU YA HALI YA HEWA NCHINI



3 **FAHAMU ZAIDI:**
HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2023



**KITAIFA**

# WATAFITI WASISITIZWA USHIRIKI JOPO LA KIMATAIFA LA SAYANSI YA MABADILIKO YA HALI YA HEWA NA TABIA NCHI

**Dar es Salaam**



Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi, Dkt. Ladislaus Chang'a aliwasisitiza watafiti mbalimbali nchini kutumia fursa zilizopo katika Jopo hilo kwa kushiriki kikamilifu na kutoa mchango wa sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa ngazi ya nchi.

Dkt. Chang'a alisema hayo wakati akizungumza na wanasayansi, watafiti, viongozi na watumishi kutoka Idara mbalimbali za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ikiwa ni moja ya mkakati wa kuhimiza na kuongeza mchango wa nchi za Afrika kwenye ripoti mbalimbali zinazotolewa na Jopo hilo la Kimataifa.



"Huu ni mkutano wangu wa kwanza kama Makamu Mwenyekiti wa IPCC nikiwa na jukumu la kuhamasisha ushiriki wa Afrika katika mchakato na kazi za IPCC, ikiwemo maandalizi ya Ripoti ya Saba. Viongozi wa sasa wa IPCC kutoka Afrika tumejipa jukumu la kuhamasisha na kuhakikisha ongezeko la ushiriki wa watafiti kutoka Afrika katika Jopo la IPCC. Aidha, niwajulishe kuwa mchakato wa ripoti hiyo, unatarajiwa kuanza hivi karibuni". Alisema Dkt. Chang'a.



Naye, Mkurugenzi wa Taasisi ya Tathmini Rasilimali, UDSM Prof. Joel Kirway alimpongeza Dkt. Chang'a kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa IPCC na kuitikia mwaliko wa kukutana na watumishi mbalimbali wa UDSM ili kuwasilisha mada ya fursa zilizopo katika Jopo la IPCC kwa Chuo cha Dar es Salaam ambacho kina Kituo cha Taaluma za Mabadiliko ya Tabianchi, kwa kutambua mchango katika maendeleo ya nchi na Afrika kwa ujumla. Aidha, baada ya majadiliano ya kina, Prof. aliahidi kutoa ushirikiano kwa kushirikisha idadi kubwa ya watumishi na wanachuo ili kuleta mabadiliko chanya katika machapisho mbalimbali ya IPCC.



## KIMATAIFA

# WADAU WAKUTANA KUJADILI MPANGO KAZI WA UWEKEZAJI WA MIUNDOMBINU YA HALI YA HEWA NCHINI

**Dodoma**




Tanzania kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Hali ya Hewa ya Denmark (DMI) kama Mshauri na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kama Taasisi ya kusimamia Utekelezaji wa mfuko (Programu) wa kuimarisha miundombinu ya hali ya hewa na ufanisi duniani kwa nchi zinazoendelea (Systematic Observations Financing facility-SOFF) iliandaa warsha ya wadau kujadili mpango kazi wa uwekezaji wa uboreshaji wa miundombinu ya hali ya hewa nchini, tarehe 21 Septemba, 2023, Dodoma, Tanzania.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC), alisema wataalamu kutoka TMA na DMI kwa ushirikiano wa pamoja wameandaa rasimu ya mpango kazi kwa kuzingatia mahitaji ya nchi na kuwakutanisha wadau ili kupata maoni ambayo yatasaidia kuboresha mpango kazi huo. Aidha, Dk.Chang'a aligusia maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa SOFF nchini, mfuko ambao umekuwa ukichangiwa na wadau mbalimbali

wa maendeleo ikiwemo Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na UNDP.

"Utekelezaji wa mradi huu nchini upo katika awamu tatu ambapo moja ya hatua za awali ni kutambua na kuainisha mahitaji ya nchi katika upande wa miundombinu ya hali ya hewa na kuandaa mpango kazi wa kushughulikia mahitaji yaliyo ainishwa ili koungeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za hali ya hewa hususani kipindi hiki ambacho tunakabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi". Alisema Dkt. Chang'a.

"Hii ni mojawapo ya hatua muhimu ambayo inaenda kuchangia katika jitihada kubwa zinazofanywa na serikali yetu ya kuimarisha huduma za hali ya hewa na kuongeza uwezo wetu wa kuhimili changamoto za mabadiliko hayo ya hali ya hewa. Tunaishukuru sana Serikali na wadau wengine wa maendeleo". Aliongezea Dkt. Chang'a.

Kwa upande wake, Mwakilishi kutoka DMI, Bw. Christian Rodrup alisema anatarajia kupokea michango muhimu kutoka kwa wadau kwa ajili ya kuboresha rasimu ya mpango kazi, pia alisisitiza kuwa kati ya nguzo nne muhimu za utoaji wa tahadhari za mapema ni pamoja na miundombinu ya hali ya hewa yenye kuweza kuchangia katika upatikanaji wa takwimu sahihi za hali ya hewa.

Naye, Mwakilishi Msaidizi wa UNDP, Tanzania, Getrude Lytuu, alisema anathamini ushirikiano uliopo baina ya wadau katika utekelezaji wa SOFF na kusisitiza Tanzania kuongeza jitihada ili kuhakikisha kuwa mpango kazi unao andaliwa unakamilishwa mapema na kwa viwango vizuri, na unawasilishwa kwa wakati katika kamati husika ili kuiwezesha Tanzania kupata nafasi kubwa ya kupewa kipaumbele cha kupewa fedha kwa ajili ya utekelezaji .



# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2023

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2023, mvua za msimu wa Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, kuna uwezekano wa ongezeko la mvua kwa baadhi ya maeneo katika wiki ya tatu na ya nne. Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi inatarajiwa hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):** | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne.** |
| **Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** | ♦ Katika kipindi hiki, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne.** |
| **Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** | ♦ Vipindi vya mvua vinavyoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.** |
| **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** | ♦ Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Oktoba,2023. |
| **Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** | ♦ Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinaweza kujitokeza katika maeneo machache.** |
| **Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** | ♦ Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. **Aidha, vipindi vya baridi vinatarajiwa kuendelea kujitokeza hususan katika maeneo ya miinuko.** |
| **Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** | ♦ Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani. **Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya nne ya mwezi.** |
| **Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma):** | ♦ Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache. **Aidha ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya nne ya mwezi.** |

# BIDHAA NA HUDUMA ZA TMA

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA KATIKA SHUGHULI ZA VIWANDA

Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania inatoa huduma za hali ya hewa zinazosaidia sekta ya Viwanda kudhibiti athari zinazohusiana na hali mbaya ya hewa. Huduma hizi zinatolewa kwa kufuata na kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

**TMA inatoa huduma zifuatazo kwa sekta ya Viwanda**

(a) Takwimu za klimatolojia kwa eneo maalum kama vile matukio ya hali mbaya ya hewa.
(b) Kasi na mwelekeo wa upepo.
(c) Utabiri mahsusi/maalum wa kisekta.
(d) Tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa ikiwemo Sunami.

**Matumizi ya Huduma zitolewazo na TMA kwa Sekta ya Viwanda**

(a) Kujua uhitaji/idadi ya bidhaa zitakazozalishwa kwa kutegemea hali ya hewa.
(b) Kupunguza uchafuzi wa mazingira.
(c) Kubuni na kuainisha madhumuni na maeneo ya kufanya ujenzi.
(d) Matumizi bora ya mashine na namna nzuri ya kutupa taka.
(e) Ubunifu katika kutengeneza na kuzalisha bidhaa;
(f) Soko kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa.
(g) Usafirishaji wa malighafi na bidhaa.








**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.